Nikuwa Talbiya (kuitika) kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kulikuwa ni: Labbaikallaahumma labbaika -Nimekuitikia ewe Mola nimekutikia, Labbaika laa shariika laka labbaika -Nimekuitikia huna mshirika wako nimekuitikia, Hakika sifa njema na neema zote ni zako pamoja na ufalme, wewe pekee usiye na mshirika

Imepokelewa kutoka kwa Abdallah bin Omari -radhi za Allah ziwe juu yake na baba yake-: "Nikuwa Talbiya (kuitika) kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kulikuwa ni: Labbaikallaahumma labbaika -Nimekuitikia ewe Mola nimekutikia, Labbaika laa shariika laka labbaika -Nimekuitikia huna mshirika wako nimekuitikia, Hakika sifa njema na neema zote ni zako pamoja na ufalme, wewe pekee usiye na mshirika.". Amesema: Na alikuwa Abdallah bin Omari akizidisha ndani yake: "Labbaika Labbaika wasa'daika, -Nimekuitikia nimekuitikia na utukufu ni wako, wal khairu biyadaika, -Na heri iko mikono mwako, na hamu zote na matendo mwisho ni kwako".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Zilikuwa talbiya (kuitika katika Hija) kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake anapotaka kuingia katika ibada ya Hija au Umra ni kusema: "Nimekuitikia ewe mola nimekuitikia" Kuitika kwa lazima kwako baada kukuitikia katika yale uliyotuita kwayo miongoni mwa ikhlasi na tauhidi na Hija na mengineyo, "Nimekuitikia, huna mshirika wako, nimekuitikia" wewe peke yako ndiye unayestahiki kuabudiwa huna mshirika wako katika uumbaji wako na uungu wako na majina yako na sifa zako, "hakika sifa njema" na shukurani na sifa "na neema" zinatoka kwako, na wewe ndiye mgawaji wake "ni zako" hugawanywa katika kila hali, "na ufalme" vile vile ni wako, "huna mshirika wako" wote ni wako wewe peke yako. Na alikuwa bin Omari radhi za Allah ziwe juu yao akizidisha katika hayo. "Labbaika wasa'daika" Nimekuitikia na utukufu ni wako, nifurahishe kwa furaha moja baada ya nyingine, "na heri iko mikononi mwako" yote, na ni kwa fadhila zako, "Nimekuitikia na shauku zote ziko kwako" na matakwa na maombi ninayaelekeza kwa yule ambaye heri iko mkononi mwake, "na matendo" ni kwa ajili yako, kwani wewe ndiye unayestahiki kuabudiwa.